



# Ndoa za Mapema na za Kulazimishwa

## Kumlazimisha mtu yeyote kuolewa ni uhalifu mbaya nchini Australia.

Nchini Australia, watu wako huru kuchagua kama wanataka kuo au kuolewa na ni nani wanayetaka kuo. Kwa kawaida, mtu lazima awe na zaidi ya umri wa **miaka 18** ili kuolewa kisheria. Katika baadhi ya mazingira mtu mwenye umri wa zaidi ya **miaka 16** anaweza kuo mtu aliye na zaidi ya umri wa miaka 18, lakini hii inahitaji amri ya mahakama.

Ni kinyume cha sheria ya Australia kumlazimisha, kumtisha au kumlaghai mtu yeyote aolewe. Pia ni kinyume cha sheria kuhimiza au kusaidia kupanga ndoa, na kushiriki katika ndoa ya lazima ikiwa wewe si mhadhiriwa. Hii inatumika kwa ndoa za kisheria, kitamaduni na kidini.

Ndoa za kukubaliana, ambapo watu wawili kwa uhuru wao wanakubali kuoana, ni tofauti na ndoa za kulazimishwa. Ndoa za kukubaliana zinakubalika kisheria nchini Australia.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, piga simu kwa polisi, nambari ya simu **000**.

Polisi nchini Australia ni salama na wanaweza kuaminika.

Ikiwa unahitaji mkalimani bila malipo piga simu kwa **131 450**.

## Ni kinyume cha sheria kuchukua au kutuma mtu kwenda nchi nyingine kufanya ndoa za kulazimishwa au kutumia mtu mwingine kupanga hii.

Wakati mwingine watu husafirishwa ng'ambo kinyume na matakwa yake au anapotoshwa kwenda ng'ambo kulazimishwa kuolewa. Hii ni kinyume cha sheria na inaweza kusababisha kufungwa gerezani.

## Je wewe, au mtu mwingine unayemjua, yuko hatarini?

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko katika hatari ya ndoa ya lazima au kuolewa mapema, unaweza kuwasiliana na **Australian Federal Police (Polisi wa Serikali ya Australia)** (AFP), nambari ya simu **131 237** (131AFP) ili kupata msaada.

AFP inaweza kukuweka salama, kutoa ushauri wa mapema na kukuelekeza kwa huduma nyingine za msaada, kama vile malazi, msaada wa kifedha, ushauri na ushauri wa kisheria na uhamiaji. Maelezo ya ziada yako kwenye **tovuti ya AFP** kwenye **www.afp.gov.au**.

## Kuna huduma nyingi nchini Australia ambazo zinaweza kukusaidia.

**My Blue Sky** ni tovuti ya taifa la Australia na laini ya msaada iliyotolewa kwa ajili ya kuzuia ndoa za lazima, kutoa maelezo, rufaa na ushauri wa kisheria bila malipo.

Piga simu kwa **(02) 9514 8115**, tuma ujumbe mfupi kwa **0481 070 844**, na utume barua pepe kwa **help@mybluesky.org.au**, au nenda kwenye **tovuti ya My Blue Sky** kwenye **www.mybluesky.org.au**

**1800RESPECT** ni huduma ya ushauri wa mzozo wa kijinsia, uhasama wa kifamilia na kinyumbani kutoka kwa taifa la Australia (Australia's national sexual assault, family and domestic violence counselling service). Hutoa maelezo na ushauri wa mtandaoni na wa simu bila malipo na wa siri. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za msaada katika eneo lako.

Piga simu kwa **1800 737 732** au nenda kwenye **tovuti ya 1800RESPECT** kwenye **www.1800RESPECT.org.au**.

## Je unahitaji mkalimani?

Piga simu kwa **Huduma ya Ufasiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS))**, nambari ya simu **131 450**. Mkalimani kutoka TIS anaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma zingine, hata hivyo TIS haitoi huduma ya ushauri. Simu zote hazilipishwi na ni za siri.

## Kwa maelezo zaidi kuhusu ndoa za kulazimishwa:

Tembelea **tovuti ya Idara ya Masuala ya Nyumbani (Department of Home Affairs)** kwenye **[www.homeaffairs.gov.au](http://www.homeaffairs.gov.au)** na utafute “ndoa za kulazimishwa” (“forced marriage”).